BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Saba – Tarehe 13 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

229. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika baadhi ya maeneo ndani ya Visiwa vya Zanzibar, kumeripotiwa kutokea matukio ya kihalifu, kwa watu kushambuliwa kwa silaha zenye ncha kali na hata kuporwa mali zao, hasa nyakati za usiku na alfajiri wanapokwenda na kurudi katika shughuli zao za kujitafutia riziki.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza matukio hayo ya uhalifu kwa maeneo yote ya Zanzibar.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

429. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kampeni ya upandaji wa miti kitaifa imewekwa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira.

(a) Je, ni miti ya aina gani inayopandwa zaidi na kwa sababu gani.

(b) Je, miti hiyo inaweza kuhimili hali ya joto katika maeneo inayopandwa.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

60. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Soko la hisa ni nyenzo muhimu katika kukuza uwekezaji, kuongeza upatikanaji wa mitaji na kuimarisha mfumo wa kifedha nchini.

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa kuanzisha soko la hisa la Zanzibar.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha soko hilo linachangia katika kukuza uchumi na uwekezaji wa ndani.

136. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wananchi wengi wanaendelea kukabiliwa na hali ngumu ya maisha kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu na huduma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia sera za kifedha na kibajeti za nchi ili kupunguza mzigo kwa wananchi wa kipato cha chini na kuhakikisha ukuaji wa uchumi unawanufaisha wananchi wote.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

456. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Kazi na Uwekezaji:

Serikali imeweka miuondombinu ya kuwavutia wawekezaji ambapo inasaidia katika ukuaji wa uchumi, licha ya hivyo, baadhi ya wawekezaji wamefunga huduma zao Zanzibar, ikiwemo Kiwanda cha Maziwa Fumba.

(a) Je, ni kitu gani kimechangia kuhama kwa muwekezaji wa Kiwanda cha Maziwa Fumba.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za ziada za kuwalinda wawekezaji wanaowekeza hapa Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

362. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ya Mhe. Dkt. Mwinyi imechukua jitihada kubwa ya kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami. Barabara ya Kiboje Uchukuni imeshatengenezwa na imefikia hatua ya kuwekwa lami, lakini bado mpaka leo haijawekwa lami.

Je, ni lini Serikali itaiweka lami barabara hiyo.

493. MHESHIMIWA MOZA MOHAMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Bandari ya Mkoani inapokea meli za mizigo kutoka sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bandari ya Tanga. Na kwa kuwa wafanyabiashara huchukua mizigo yao na kuilipia bila ya kuwepo na utaratibu maalumu wa malipo na hata bila ya kupewa risiti za kielektroniki.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inapanga malipo ya bei za bidhaa wanazoziingiza wafanyabiashara kupitia Bandari ya Mkoani.

(b) Ni lini Serikali itahakikisha kila mfanyabiashara anapatiwa risiti za kielektroniki wakati wa malipo ya mizigo.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

399. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kwa kuwa hivi sasa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano imekuwa sana na wahalifu wa mitandao wamekuwa wakiitumia kufanya vitendo vya uhalifu ikiwemo udukuzi wa mitandao, huku ikihitajika kusomesha vijana wetu waweze kupambana na uhalifu huo.

(a) Je, Serikali imeweka mpango gani wa kusomesha wataalamu wa fani mbalimbali za TEHAMA ikiwemo Akili Unde (A.I)

(b) Je, kuna wataalamu wangapi hivi sasa wa kutengeneza mifumo ya huduma, na kila mwaka inapangwa bajeti ya kiasi gani kusomesha wataalamu zaidi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

366. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali imechukua jitihada kubwa za kuimarisha mabonde ya mpunga katika Jimbo la Uzini, lakini bado kuna changamoto ya uvamizi wa maeneo ya kulima mpunga katika maeneo hayo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inadhibiti suala hili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

381. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kuimarisha ubora wa elimu ya msingi nchini.

430. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Utoaji wa vyeti kwa vijana wanaomaliza skuli, ni ishara ya utambulisho wao.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuondolewa kwa vyeti vya Kidato cha Pili (Form II).

**Wizara ya Afya:**

33. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Madaktari bingwa wa zamani waliostaafu wamefanyakazi kubwa kwa uzalendo mkubwa wakati wao wakitoa huduma za afya Zanzibar. Hata hivyo, Madaktari hao hivi sasa wamekuwa na wakati mgumu katika maisha kwa vile pencheni wanayolipwa ni ndogo ukilinganisha na kuongezeka kwa gharama za maisha.

(a) Je, ni hatua gani Serikali itachukuwa kuhakikisha Madaktari bingwa wastaafu wanaongezewa pencheni zao ili kukidhi hali ya ongezeko la gharama za maisha.

(b) Kwa kuwa hivi sasa kuna ongezeko la hospitali nyingi katika kila Wilaya, je, Serikali inao mpango wa kutumia uzoefu wa Madaktari wastaafu katika ushauri na uzoefu katika uendeshaji wa hospitali hizo.

205. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ujenzi wa Kituo cha Afya Ukutini Pemba umesimama kwa takribani miezi mitano sasa, hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi waliokuwa wakipata huduma katika Kituo hicho.

(a) Ni mkandarasi gani aliyepatiwa zabuni ya ujenzi huo na kwa gharama ya kiasi gani.

(b) Ni kwa namna gani Serikali inafahamu kusimama kwa mradi huo na kuchelewa kumalizika kwa wakati.

(c) Ni ipi ahadi ya Serikali kwa wananchi wa Ukutini katika kumalizika kwa ujenzi huo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

143. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tatizo la uvuvi haramu bado linaathiri rasilimali za bahari na kipato cha wavuvi halali.

Je, Wizara inachukua hatua gani madhubuti kudhibiti na kulinda rasilimali za bahari.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

244. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mamlaka ya Mji Mkongwe imekuwa ikifanya vizuri sana katika kuhifadhi *Tangible Preservation* (Uhifadhi Unaoonekana) ndani ya Mji Mkongwe, kwa maana ya majengo kupitia programu mbalimbali hususani ya ukarabati wa majengo ya Mji Mkongwe, chini ya ufadhili wa Serikali kupitia fedha za ndani.

(a) Je, ni ipi mikakati ya Mji Mkongwe katika kuhifadhi *Non-Tangible Preservation* (Uhifadhi Usioonekana), kama vile tamaduni za Kizanzibari ndani ya Mji Mkongwe.

(b) Je, ni ipi mikakati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe katika kuhifadhi *Non-Tangible Preservation* (Uhifadhi Usioonekana) pale wanapohamishwa wakaazi wa awali wa Mji Mkongwe, baada ya Mamlaka kufanya ukarabati wa majengo na kuletwa wakazi wengine kwa sifa ya ushindani wa bei.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

464. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Moja ya sehemu ya kiashiria hatarishi katika mikataba ni wakati panapojitokeza mabadiliko ya mkataba *(Adendum of the Contract).*

(a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inajiridhisha uhalali wa gharama za mkataba wakati zinapowasilishwa kabla ya malipo.

(b) Je, ni mikataba mingapi Serikali imefanya mabadiliko ya gharama *(Adendum)* wakati wa utekelezaji wa mikataba ya asili.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**13 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR